



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. NDC/I.20/6/VOL.VII/143

15/11/2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia **nafasi 1** za kazi na anakaribisha maombi kwa watazania wote wenye sifa na uwezo, kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi kama ilivyo orodheshwa katika tangazo hili. Aidha mnajulishwa kuwa mwisho wa maombi haya ni tarehe **29/11/2021**.

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – (NAFASI 1)

a) Sifa za mwombaji.

Mwenye elimu ya kidato cha nne au sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti katika moja ya fani zifuatazo. Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

b) Kazi na majukumu

- Afisa masuuli na mtendaji Mkuu wa Serikali za Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na kamati za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia sera, Sheria na taratibu.
- Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.

- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Mweñyekiti wa kikao cha wataamu waliopo katika Kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo ndogo za Kijiji.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

2. MAELEKEZO

- Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hawapungui umri wa miaka 18.
- Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) zenye wadhamini wawili na mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.
- Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI,
- Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
 - Astahhada/Cheti cha utaalamu kulingana na sifa za nafasi husika.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita.
 - Cheti cha kuzaliwa.
 - Picha mbili za passport size.
- Hati ya matokeo ya kidato cha nne/sita (Result slip) na "Transcript" hazitafanyiwa kazi.
- Watumishi wa Umma walioajiriwa wapitishie maombi yao kwa waajiri wao.
- Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la mtihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya ufundi la Taifa (NACTE).

- x. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 29/11/2021 saa 9:30 alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakapo chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.njombedc.go.tz na kwenye mbaao za matangazo za Halmashauri.

Barua zote zitumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,
S.L.P 547,
NJOMBE.

Tangazo hili limetolewa na:-



Sharifa Y. Nabalang'anya
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NJOMBE

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
NJOMBE